# "SABATO"

KWA NINI WEWE KAMA MKRISTO HUPUMZIKI SIKU YA SABATO?

NA
FRANCIS WACHESA

Neno Sabato ni neno ambalo wengi wameshindwa kulielewa. Watu wengine wanasema ya kwamba Sabato ni Jumapili au siku ya kwanza ya juma. Lakini sivyo lilivyo. Kama Sabato si Jumapili basi ni siku gani?

Sabato ni siku ya saba. Mungu aliviumba vitu vyote katika siku sita, siku ya saba akapumzika. Ndiyo jumamosi katika kalenda ya Kiswahili. "Basi mbingu na nchi zikamalizika na jeshi lake lote; na siku ya saba mungu akamaliza kazi yake yote aliyoifanya, akastarehe siku ya saba akaacha kufanya." Mwa. 2:1-2.

Mungu alistarehe baada ya kumwagiza mwanadamu kuvitiisha na kula matunda ya Edeni. Kwa sababu hiyo Adamu, Nuhu na Ibrahimu hawakuitunza Sabato kwa sababu hatuoni mfano wo wote katika neno la Mungu. Adamu na Hawa waliamriwa kufanya kazi, hakuna agizo la kuitunza siku ya saba "Sabato". "Bwana" Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika Bustani ya Edeni, ailime na kuitunza. (Mwa. 2:15) Nuhu, Ibrahimu, Isaka na Yakobo (Aliyeitwa baadaye Israeli.) hawakupewa amri ya kustarehe siku ya saba. Sasa swali linabaki, basi, Sabato walipewa nani? Katika kitabu cha Kutoka Bwana anamwagiza Musa anene na wana wa Israeli, "Bwana akasema na Musa na kumwambia, kisha nena wewe na wana wa Israeli na kuwaambia, hakika mtazishika Sabato zangu, kwa kuwa ni ishara kati ya mimi na ninyi, katika vizazi vyenu vyote; ili mpate kujua ya kuwa mimi ndimi bwana niwatakasaye ninyi. Basi mtaishika hiyo sabato kwa kuwa ni takatifu kwenu, kila mtu atakayeitia unajisi hakika yake atauawa, kwa kuwa kila mtu afanyaye kazi katika siku hiyo nafsi hiyo itakatwa mbali na watu wake. Kazi itafanywa siku sita, lakini siku ya saba ni Sabato ya kustarehe kabisa, takatifu kwa bwana kila mtu atakayefanya kazi yo yote katika siku ya sabato hakika atauawa." Kutoka 31:12-15. Wana wa Israeli walipopewa sheria ndipo walipojulishwa Sabato takatifu walipofika Mlima Sinai. "Ulishuka juu ya mlima Sinai na kusema nao toka mbiguni, ukawapa hukumu za haki na sheria za haki na sheria za kweli , na amri nzuri na maagizo. Ukawajulisha Sabato yako takatifu, na kuwaagiza maagizo na amri na sheria kwa mkono wa mtumishi wako Musa. (Neh. 9:13-14). Mungu alitoa Sabato kwa wana wa Israeli kuwa kama ishara kati yao na yeye. "Kisha nena wewe na wana wa Israeli na kuwaambia hakika mtazishika Sabato zangu kwa kuwa ni ishara kati ya mimi na ninyi...." (Kut. 31:13; Eze. 20:12).

Kwa nini Mungu aliwapa wana wa Israeli Sabato (siku) ya kupumzika? Kwa sababu walikuwa watumwa katika nchi ya Misri katika bara la Afrika. "Nawe utakumbuka ya kuwa ulikuwa mtumwa katika nchi ya Misri na kuwa Bwana Mungu wako, alikutoa huko kwa mkono ulionyoshwa, kwa sababu hiyo Bwana Mungu wako alikuamuru uishike Sabato. (Kumbukumbu 5:15). Kwa sababu hiyo watu wasio wana wa Israeli hawakupewa sheria ya Sabato kwa sababu hawakuwa Mlima Sinai na tena hawakuwa watumwa katika nchi ya Misri. Je, Waisraeli hadi leo wangali wanashurutishwa kuitunza Sabato?

Sabato ilikoma Yesu alipokuwa msalabani. "Akisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iyokuwa na uadui kwetu; Akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea msalabani, akiisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo. Basi, mtu asiwahukumu (kuwashurutisha) ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato, mambo hayo yalikuwa kivuli cha mambo yajayo, bali mwili ni Kristo." Kol. 2:14-17. Nabii Hosea alitabiri kuhusu siku hiyo kuondolewa kwa sikukuu zake na siku zake za mwandamo pamoja na Sabato. "Tena nitaikomesha furaha yake yote, na sikukuu zake, na siku zake za mwandamo wa mwezi, na Sabato zake, na makusanyiko yake yote yaliyoamriwa." Hosea 2:11. Unabii wa Hosea ulitimilika wakati Yesu Kristo Mwana wa Mungu wa pekee alipokuwa msalabani. "Hapo ilikuwa yapata saa sita, kukawa giza juu ya nchi yote hata saa kenda." Luka 23:44.

Katika kitabu cha Waebrania, Sabato inayozungumziwa hapa ni starehe inayowasubiri wakristo waaminifu kule mbiguni. Hakutakuwa na kufanya kazi kwa wale watakaokwenda mbinguni. "Basi ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope mmoja wenu asije akaonekana ameikosa. Maana ni kweli sisi nasi tumehubiriwa habari njema vile vile kama hao. Lakini neno lile lililosikiwa halikuwafaa hao (wana wa Israeli). Kwa sababu halikuchaganyika na imani ndani yao waliosikia, maana sisi tulioamini (Wakristo) tunaingia katika raha ile, kama vile alivyo sema. Leo kama mkisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu, maana kama Yoshua angaliwapa raha (Sabato) asingenena siku nyingine baadaye. Basi, imesalia raha ya Sabato kwa watu wa Mungu, kwa maana yeye aliyeingia katika raha amestarehe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake." Waebrania 4:1-10. Katika mstari wa tisa unazungumzia matumaini ya starehe kwa watu wa Mungu (Wakristo waaminifu). Mstari huu hauna maana kuwa starehe ni hapa duniani. Starehe ya hapa duniani ni katika Kristo Yesu Bwana wa Sabato. "Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha." Mathayo 11:28.

Mtu akiwa nje ya Kristo yeye ni mtumwa wa Shetani, hana siku ya kupumzika, anamfanyia Shetani kazi kama vile wana wa Israeli walivyowafanyia kazi Wamisiri. Basi njoo kwa Yesu umpokee kama Bwana na Mwokozi wa maisha yako. 1) Kumwamini: "Kwa hiyo naliwaambieni ya kwamba mtakufa katika dhambi zenu kwa sababu msiposadiki ya kuwa mimi ndiye mtakufa katika dhambi zenu." Yohana 8:24. 2) Kutubu: "....Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu...." Matendo 2:38. 3) Kumkiri Kristo: "Akajibu akanena, naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu." Matendo 8:37. 4) Na kubatizwa kwa ondoleo la dhambi zako: "Aaminiye na kubatizwa ataokoka asiyeamini atahukumiwa." Marko 16:16. Na Bwana mwenyewe atakuongeza kwenye kanisa lake. "Wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote, Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa." Matendo 2:47.

**www.kanisalakristo.com**